

TANGAZO LA SERIKALI NA la tarehe

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MANISPAA)
YA MWAKA, 1982**

(Na. 8 ya 1982)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu Na. 89.

**SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
(ULINZI WA UMMA) ZA MWAKA 2017**

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za Jina Halmashauri ya Manispaa ya Musoma (Ulinzi wa Umma) za mwaka 2017 Zitatumika katika eneo lote la Manispaa ya Musoma na zitaanza kutumika baada ya kusainiwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Jinan a matumizi

2. Katika sheria hizi:-
“Manispaa” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
“Mkazi” maana yake ni mtu yeyote anayeishi ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Tafsiri

“Kaya” maana yake mume, mke, watoto na mtu yeyote anayeishi kumtengemea Mkuu wa Kaya au hata mtu mmoja anayeishi peke yake na kujitegemea.

3. Kila mkazi Mwenye umri usiopungua miaka 18 atawajibika kushiriki katika ulinzi wa umma kama utakavyoratibiwa na uongozi wa Mtaa, Kijiji au kitongoji kwa usimamizi wa Ulinzi wa kamati ya Maendeleo ya Kata. Wajibu wa Kushiriki au kuhesabika kuwa umeshiriki

4. Kila Mkazi atahesabika kuwa ametekeleza kifungu cha 3 hapo juu iwapo atafanya yafuatayo:-
 - (i) Atashiriki ulinzi yeye mwenyewe kwa mujibu wa utaratibu utakokuwa umepangwa na uongozi wa mtaaa, Kijiji au Kitongoji kwa usimamizi wa Kamati ya Maendeleo ya Kata.

- (ii) Iwapo kaya yake itachangia kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Kamati ya Mtaa, Halmashauri ya Kijiji au Kitongoji, kutegemeana na hali halisi kwa ajili ya kugharamia shughuli za ulinzi, kukodisha kampuni ya ulinzi ya binafsi, kununua vifaa vya ulinzi kama tochi, betri, mishale, pinde, filimbi, sare n.k

- | | | |
|----|---|----------------------------------|
| 4. | Kutaanzishwa kikundi cha ulinzi katika kila Mtaa, Kijiji au Kitongoji katika Manispaa. | Kikundi cha ulinzi |
| 5. | Kila kikundi cha ulinzi kitakuwa na kiongozi wake atakaye tambulika kama kamanda wa kikundi. | Kiongozi wa kikundi |
| 6. | Kila Kamanda wa kikundi atatakiwa kuwa na orodha ya wakazi wate wanaostahili kushiriki katika ulinzi katika Mtaa, Kijiji au Kitongoji na hiyo itahifadhiwa katika daftari maalum kwa kazi hiyo. | Orodha ya wakaazi |
| | Kamanda wa kikundi cha ulinzi na makamanda wasaidizi watawajibika kusimamia kila kikundi kitakachokuwa zamu kwa siku husika. Kila kamanda Msaidizi atawajibika kuwasilisha orodha ya walinzi waliopo zamu ya ulinzi ya kila siku kwa kamanda wa kikundi ambaye naye atawasilisha orodha hiyo kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi kilicho karibu. | Wajibu wa kamanda kusimamia zamu |
| | Ni marufuku mtu yeyote kutoshiriki katika ulinzi, kushawishi mwingine asishiriki ama kumsaidia mwingine kukwepa kushiriki katika ulinzi ndani ya Mtaa, Kijiji au kitongoji kingine katika Manispaa. | Makoasa |
| | Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyumbe na Kifungu chochote cha sheria ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana atatozwa faini isiyopungua Shs. 200,000/= au kifungo chake ni miezi kumi na miwili (12) jela au vyote kwa pamoja. | Adhabu |

Muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma umebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kufatia azimio la Mkutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehe mwezi 2017 mbele ya :-

.....
MH. PATRICK WILLIUM GUMBO
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA.

.....
FIDELICA MYOVELLA
MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA

NAKUBALI,

TAREHE
DODOMA

.....
MH. GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI